**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KAGERA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA SERIKALI YA KITUNTU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI YA MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KAGERA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE**

**Mkuu wa Shule - 0784000131**
**Makamu Mkuu wa Shule - 0784990418**
**Mwalimu wa nidhamu - 0766531449**
**Mwalimu wa Taaluma- 0683152501**

**Shule ya Sekondari KITUNTU**

**S.L.P 486**

**Tarehe ………….**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ......................................**

**..................................................................................**

**S.L.P .........................................................................**

**..................................................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KITUNTU HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE MKOA KAGERA MWAKA ……..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **…….** na atasoma tahasusi atakayochaguliwa kati ya HKL na PCM. Ni shule ya mchanganyiko yaani Wavulana na Wasichana.

Shule ya Sekondari Kituntu ipo umbali wa Kilometa 11 Kaskazini Mashariki mwa Mji wa Kayanga.Usafiri wa basi kutoka mjini Bukoba - Karagwe unapatikana kwa shilingi 5,000. Aidha kutoka Kayanga Mjini kwenda Kituntu sekondari ni shilingi 3000 utapanda tax za kuelekea Rwambaizi na utashuka Kituntu sekondari ipo barabarani.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe ............, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ................. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule kwa wavulana.**

i. Sare ya shule hii kwa wanafunzi wa kidato cha Tano ni Suruali 2 nyeusi (zisiwe modal na ziwe na turn up)
ii. Mashati 2 meupe mikono mirefu.
iii. Sare ya Michezo ni truck suit moja rangi ya blue yenye michirizi miwili nyeupe.( Zinapatikana karibu na shule kwa pamoja kuondoa utofauti wa rangi)
iv. raba .
v. Viatu vya shule ni vyeusi pair 2 vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
vi. Soksi jozi mbili nyeusi.
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali. ( usiwe na chuma)
viii. Sweta moja rangi ya kijivu . .(Zinapatikana karibu na shule kwa pamoja kuondoa utofauti wa rangi)
ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali 2 .
x. T-shirt 1 rangi ya kijani jeshi yenye kola. (Zinapatikana karibu na shule kwa pamoja kuondoa utofauti wa rangi)

xi. Tai moja yenye michirizi mikubwa nyeupe na kijani .(Zinapatikana karibu na shule kwa pamoja kuondoa utofauti wa rangi)

xii. Tisheti (T-shirt) moja ya shule ya kuvaa siku ya Jumatano rangi ya light blue yenye kola shingoni. (Zinapatikana karibu na shule kwa anakayehitaji)

**2.2. Sare za shule kwa wasichana.**

i) Sketi 2 rangi nyeusi zenye Malinda yenye michirizi miwili nyeupe mbele.
ii) Shati 2 nyeupe yenye mikono mirefu.
iii) Sare za michezo ni truck suit moja rangi ya blue yenye michirizi nyeupe pembeni. (Zinapatikana karibu na shule kwa pamoja kuondoa utofauti wa rangi)
iv) Stocking pair 2 nyeupe.
v) Sweta moja rangi ya kijivu.( Zinapatikana karibu na shule kwa pamoja kuondoa utofauti wa rangi)
vi) Nguo za kushindia ( shamba dress) gauni rangi ya kijivu. (Mshono wa solo)
vii) Tai moja yenye rangi nyeupe na kijani. .(Zinapatikana karibu na shule kwa pamoja kuondoa utofauti wa rangi)
viii) T-shirt moja ya shule ya kuvaa siku ya Jumatano rangi ya light blue yenye Kola shingoni. (Zinapatikana karibu na shule kwa pamoja kuondoa utofauti wa rangi)

**2.3. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 8 aina ya counter books 3 quires.
ii. **Ream mbili (A4)** za Karatasi. Leta ream moja kila muhula.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi uliyochaguliwa kati ya HKL na PCM orodha imeambatanishwa.
iv. Godoro lenye vipimo vya 2.5X6
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya kijani, blanket 1, foronya ya godoro 1 lenye cover ya rangi ya damu ya mzee, chandarua 1 rangi nyeupe ya duara.
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani ya chuma, bakuli, kijiko na kikombe chenye ujazo wa nusu Lita.

viii. Ndoo 2 za lita 20 zenye mifuniko.
ix. Kwanja 1 (Wasichana), jembe 1 (Wavulana) , reki 1, mifagio 1 wa ndani soft bloom na 1 nje aina ya chelewa.
x. Sanduku la mbao au chuma na kofuli
xi. Aje na vifaa vya usafi binafsi Sabuni, mafuta ya kujipaka, mswaki, dawa ya meno, dawa ya viatu , brush na Kandambili.
xii. Njoo na Tochi ila Mishumaa ni marufuku.
xiii. Scientific calculator function moja (991) kwa wanafunzi wa Mchepuo wa PCM.

## 2.4. Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000.00 ( Kila mwaka) |
| 2 | Tahadhari | 5,000.00 |
| 3. | Nembo | 5,000.00 |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000.00 |
| | **Jumla** | **80,000.00** |

**N.B Malipo haya yalipwe akaunti ya shule namba 31901100016 jina la akaunti REVENUE COLLECTION ACCOUNT KITUNTU.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule kwa Msiba au Ugonjwa tu.**
- **Mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya kwa ajili ya matibabu ya afya yake. Shule haitoi matibabu yoyote kwa mwanafunzi. Huduma ya matibabu ni jukumu la mzazi.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Nakala ya Matokeo ya kidato cha NNE kutoka Necta mwaka 2024.
vi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KITUNTU**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

......................................

**Jina la Mkuu wa Shule MUGANYIZI A. KATATUMBA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 07629663731 AU 0784000131**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0784990418**
- **Mwandamizi Taaluma 0683152501**
- **Mwandamizi Malezi 0766531449**

**SHULE YA SEKONDARI KITUNTU**
**FOMU YA KUKUBALI NA KUTII SHERIA ZA SHULE**

ANWANI...................................................................................................

Mimi............................................................... (Jina la mwanafunzi) nimepokea barua ya kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Kituntu kuanzia tarehe ……….. hadi ……. Nakubali nafasi hiyo kwa moyo mkunjufu. Baada ya kusoma na kuelewa sheria za shule, naahidi kuwa nitatii sheria hizo kama zilivyoainishwa katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Kituntu Endapo nitashindwa kutii sheria hizo hatua inayostahili ichukuliwe dhidi yangu

Natoa ahadi hii mbele ya Mzazi /mlezi wangu ambaye ametia sahihi yake hapa chini.

Jina la mwanafunzi .......................................... sahihi...........................................

Mimi............................................................... (Jina la mzazi /mlezi) ambaye ni mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, nakubali mwanangu ajiunge kidato cha Tano katika shule ya Sekondari Kituntu na kutii sheria za shule na naahidi kushirikiana na shule ili kuhakikisha tunatoa malezi bora kulingana na sheria hizo na nyingine ambazo hazikutajwa pia.

Iwapo sitakuwepo mimi likitokea tatizo ninaweza kuwakilishwa na

1.................................................... ambaye ni...........................................

2....................................................... ambaye ni.................................................

(Eleza uhusiano wako na wawakilishi hao).........................................................

Sahihi.....................................................

Tarehe............................................................

**SHULE YA SEKONDARI KITUNTU**
**KIAMBATANISHO B**
**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. JINA KAMILI...................................................... (Kama ilivyo kwenye Selform)

2. Tarehe ya kuzaliwa...................................................

3. Mahali alipozaliwa: Wilaya...................Kijiji................ Kata.........................

4. Anwani ya nyumbani ni...................................................

5. Dini yake.................................................................

**WAZAZI**/MLEZI

Jina ….................................... Anwani................................................

Anaishi /Amefariki (kata isiyohusika)..................................................

Ni raia wa nchi ipi? Itaje................................................ (Tanzania/nchi nyingine)

**MAELEZO YA AFYA**

Eleza kama una tatizo lolote linalohitaji msaada au linaloweza kuathiri utendaji wako wa kazi za kila siku pamoja na maendeleo yako ya masomo. Maombi maalumu yadhibitishwe na daktari.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

........................................................................................................

**SHULE YA SEKONDARI KITUNTU**
**KIAMBATANISHO C**
**HATI YA UTHIBITISHO WA TABIBU (anayetambuliwa na serikali)**

Nathibitisha kwamba nimemchunguza mwanafunzi

Jina: .........................................................

Kinyesi....................... Matokeo.........................................................

Mkojo..................... Matokeo.........................................................

Macho..................... Matokeo.............................................

Damu..................... Matokeo.............................................

Mapigo ya moyo..................... Matokeo.............................................

Urine Pregnancy Test (UPT)..................... Matokeo.............................................

Matatizo mengine kama yapo.....................

**MATIBABU** Yafuatayo yametolewa (kama ni ugonjwa wa kudumu eleza)

....................................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................................

..............................................................................................................................

Jina la tabibu: .........................................................Sahihi: .....................................

Tarehe..............................................................

Muhuri.............................................................

# OORODHA YA VITABU MUHIMU KWA KILA SOMO

Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma. Orodhaya vitabu vinavyotakiwa kwa kila idara ni kama ifuatavyo:-

**ADVANCED LEVEL PCM BOOKS REQUIRED**

| SUBJECT | BOOK TITLE |
|---|---|
| BASIC MATH'S | 1. A-level math's form 5 (TIE)<br>2. A-Level math's form 5 (TRANTA)<br>3. Septin sillem form 5 (MAYOMBYA)<br>4. Advanced math's class xi- S.chads |
| PHYSICS | 1. A- level physics form 5 (S.CHAD'S xi)<br>2. A-Level physics (NELKON)<br>3. A-Level physics form 5 (TIE) |
| CHEMISTRY | 1. Ramsden A-level chemistry<br>2. A-level chemistry (S. CHAD'S xi)<br>3. General chemistry form 5 and 6 (TIE)<br>4. Physics chemistry form 5 and 6 (TIE)<br>5. Organic chemistry form 5 and 6 (TIE)<br>6. Inorganic chemistry form 5 and 6 (TIE) |

**ADVANCED LEVEL HKL BOOKS REQUIRED**

| SUBJECT | BOOK TITLE |
|---|---|
| **HISTORY** | 1. Essential in Advanced Level History paper 1 .By Salah Yssin (2010)<br>2. Essential in Advanced Level History paper 2.By Salah Yassin (2010).<br>3. Advanced History for secondary schools form five. By Tanzania institutes ofEducation (2022)<br>4. Advanced History for secondary schools form six. By Tanzania Insitute of Eduction (2022).<br>5. A revised History for Advanced level and Colleges Part one. By Nassoro Hbib Mbwana Msonde.<br>6. Mastering Advanced History Book one .By Kato. A. Kassim. |
| **KISWAHILI** | 1. Nadharia ya lugha ya Kiswahili kidato cha tano na sita ;Nyambari Nyangwine na Masebo2021<br>2. Sarui maumbo y,x, wahili sarufi (SAMAKISA)Sekondari na vyuo-Kihore Y,M na Massamba ,D.P.B TUKI (2003)<br>**3.** Kamusi ya Kiswahili sanifu ,Toleo la pili English –swahili Dictionary – TUKI. |

| | |
|---|---|
| **FASIHI** | 1. Nadharia ya fasihi kidato cha tano na sita Masebo- Oxfoprd university Press.<br>2. Tahakiki vitabu teule vya Kiswahili kidato cha 5 NA 6 Nyambari Nyangwine na Masebo |
| **RIWAYA** | 1. Mfadhiri – Hussein Tuwa<br>2. Usiku Utakapokwisha – Mbunda Msokile<br>3. Kufikirika – Shaaban Robert<br>4. Vuta nikuvute – Shafi A. Shafi |
| **TAMTHILIYA** | 1. Kwenye ukingo wa Thim – Ebrahim Hussein<br>2. Moran – Emmanuel Mbogo<br>3. Kivuli Kinaishi – Said Mohamed<br>4. Nguzo Mama – Penina Mhando |
| **USHAIRI** | 1. Chungu Tamu – Theobald Mvungi<br>2. Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu<br>3. Mapenzi bora – Shaaban Robert<br>4. Kimbunga – Haji G. Haji |
| **ENGLISH** | 1. Macmillan Education Ltd. 2000, Encounters from Africa, Macmillan<br>2. Ayi Kwei Amah, 1996, The Beautifulones are not yet born, EAEP<br>3. Chinua, Achebe, 1991, A Man of thepeople, BAEP<br>4. Ndunguru 1999, Divine providence,Mkuki na Nyote<br>5. Magala Nyago, 1985,The Rape pf thepearl<br>6. Namige Kayondo, 1995 VanishingShadows, Macmillan<br>7. Danny Sato, 1983, His Excellency theHead of State, Macmillan<br>8. David Omowale, 2002, A season ofwalting, EAEP<br>9. Fransis Lubuga, 1990, Betrayel in thecity, Heinemann<br>10. Ngungi wa Thiong'o, et al 1982, I will marry when I want, EAEP<br>11.Bukenya, 1984, The Bride, EAEP<br>12. Okot Omitah 1991, LwandaMegere Heinemann<br>13.Henrik Ibsen, 1974, An Enemy of thepeople, Eyre |

| | |
|---|---|
| | Matheuen<br>14.John Ruganda 2005, Black Mamba, EAEP<br>15.Charles Mloka, 2002, The wonderful surgeon and other poems, Mkuki na Nyota<br>16.Tanzania institute of Education, 1996, selected poems, print pak (T) Limited.<br>17.The real English textbook Advancedlevel, Dr.kadeghe Michael |